**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA KATIBA NA SHERIA**

# TAARIFA KWA UMMA

Wizara ya Katiba na Sheria kwa mujibu wa Kanuni za Ithibati za Waendesha Maridhiano, Majadiliano, Upatanishi na Usuluhishi zilizotangazwa kwa Tangazo la Serikali Na. 147/2021 (Reconciliation, Negotiation, Mediation and Arbitration (Practisioners Acrediation Regulations, GN No. 147/2021) imepewa mamlaka ya kutoa ithibati kwa Waendesha Maridhiano, Majadiliano, Upatanishi na Usuluhishi ambao wanakidhi vigezo kwa mujibu wa Kanuni husika.

Hivyo, Wizara inapenda kuwatangazia watu wenye nia ya kutoa Huduma za Usuluhishi, Maridhiano, Majadiliano na Upatanishi ambao wanakidhi vigezo kwa mujibu wa Kanuni; kuwasilisha maombi yao pamoja na kuambatisha nyaraka kwenye Portal ya **HAKI SHERIA**(***https://tlegalaid.sheria.go.tz***)***.*** *Kwa mwombaji mpya ingia eneo la* ***MTATUZI WA MIGOGORO*** *kisha bonyeza* ***Sajili.*** Kwa ufafanuzi zaidi tafadhali wasiliana na Ofisi ya Msajili kupitia ***msajili.mmuu@sheria.go.tz*** au simu namba ***0714237904.*** Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 09 Januari, 2026. Imetolewa Na,

**KITENGO CHA MAWASILIANO SERIKALINI**

**WIZARA YA KATIBA NA SHERIA**

**27 Novemba, 2025**